# KATIBA

# YA

# UMOJA NI NGUVU

*IMETAYARISHWA NA UMOJA NI NGUVU NA KUPITISHWA*

TAREHE ................................................

# UMOJA NI NGUVU
# HATI YA KUPITISHA KATIBA

1. Sisi tulioorodhesha majina yetu hapa chini na kuweka sahihi zetu mbele ya majina yetu leo tarehe......................Mwezi....................Mwaka..................Saa................ Tukiwa wajumbe wa mkutano mkuu wa Umoja ni Nguvu uliofanyika Mbezi Luis Kwa.....................................................................................................................

   Tumeamua kupitisha katiba hii ya Umoja ni Nguvu.

2. Kwamba katiba hii imetokana na utashi pamoja na mawazo yetu sisi wenyewe, hivyo tukiwa na akili timamu tumeielewa na tumekubali iwe dira yetu katika shughuli zote zinazohusu umoja wetu, daima tutaiheshimu na kuilinda.

| JINA | SAHIHI | TAREHE |
|---|---|---|
| 1. Bw. Adam .M. Kiheka | | 14/11/2010 |
| 2. Bw. Avitus J. Rwezaula | | 14/11/2010 |
| 3. Bw. Joseph S. Kufulu | | 14/11/2010 |
| 4. Bw. Respicius D. Rutha | | 14/11/2010 |
| 5. Bw. Barthazari T. Mangashi | | 14/11/10 |
| 6. Dr. Santos H. Lyando | | 14/11/2010 |
| 7. Dr. Boniventure E. Mbanile | | 14/11/2010 |
| 8. Bw. Daniel D. Malimi | | 14/11/10 |
| 9. Bw. Andrew M. Daudi | | 14/04/10 |
| 10. Bw. Celsus R. Dibogo | | 14/11/2010 |
| 11. Bibi Zainabu R. Bakari | | 14/11/2010 |
| 12. Bw. Killian .K. Chuma | | 14 Nov 2010 |
| 13. Bw Slylivester G. Satu | | 14/11/2010 |
| 14. Bw. Yohana I. Napake | | 14/11/10 |
| 15. Bw.Robert E. Lukuka | | 14/11/10 |

# ORODHA NA MPANGILIO WA IBARA.

## SEHEMU YA KWANZA


| | |
|---|---|
| **Utangulizi:** | **MSINGI WA KATIBA** |
| **Ibara ya 1:** | **TAFSIRI YA MANENO** |
| (a) | Maafa |
| (b) | Mtoto |
| ( c ) | Wategemezi |
| (d) | Mlezi |
| (e) | Mwanakikundi |
| **Ibara ya 2:** | **UTAMBULISHO** |
| (a) | Jina la Kikundi |
| (b) | Makazi ya Kikundi |
| ( c) | Anuani ya Posta. |
| | **SEHEMU YA PILI** |
| **Ibara ya 3:** | **MADHUMUNI** |
| (a) | Kusaidiana katika matatizo |
| (b) | Kushirikiana katika mambo mengine. |
| **Ibara ya 4:** | **MISIBA INAYOSTAHILI MISAADA** |
| (a) | Mwanakikundi |
| (b) | Mke/Mume wa Mwanakikundi |
| (c) | Watoto wa mwanakikundi |
| (d) | Baba/ Mama au Mlezi wa mwanakikundi walioanishwa katika fomu ya Mwanakikundi. |
| (e) | Wategemezi wa mwanakikundi. |
| **Ibara ya 5:** | **AINA ZA MISIBA** |
| (a) | Misiba tofauti |
| (b) | Msiba mmoja mwanakikundi tofauti |
| (c) | Misiba mingi mwanakikundi mmoja |
| (d) | Misiba mingi wakati tofauti |
| (e) | Misiba mingi sehemu tofauti. |

Ibara ya 6: MIPAKA YA KUSAIDIANA KATIKA UGONJWA.
(a) Mgonjwa aliyelazwa hospitalini
(b) Mwanakikundi mgonjwa.

Ibara ya 7: MIPAKA YA KUSAIDIANA KATIKA MAAFA

SEHEMU YA TATU

Ibara ya 8: WANAKIKUNDI
(a) Sifa za wanakikundi
(b) Ada kama sharti la mwanakikundi
(c) Mwanakikundi mpya.
(d)

Ibara ya 9: HAKI YA MWANAKIKUNDI
(a) Haki ya kusaidiwa
(b) Haki ya kukagua kumbukumbu
(c) Haki ya kupewa maelezo
(d) Haki ya kuongoza
(e) Haki ya usawa.

Ibara ya 10: WAJIBU WA MWANAKIKUNDI
(a) Kulipa ada
(b) Kulipa michango mingine
(c) Wajibu wa kushirikiana
(d) Wajibu wa kulinda katiba
(e) Siri ya kikundi

Ibara ya 11: KUJIONDOA AU KUVULIWA UANAKIKUNDI
(a) Kujiondoa mwenyewe
(b) Kuhamia nje ya Dar Es Salaam
(c) Kifo cha mwanakikundi
(d) Kukiuka katiba
(e) Haki ya fedha ya mwanakikundi

Ibara ya 12: MUDA NA KIWANGO CHA MSAADA
(a) Muda wa kutoa msaada
(b) Kiwango cha msaada

SEHEMU YA NNE

Ibara ya 13: ADA NA MICHANGO
(a) Ada ya kiingilio
(b) Ada ya kila mwezi
(c) Ada nyinginezo

| | | |
|---|---|---|
| **Ibara ya 14:** | | **HAZINA** |
| | (a) | Udhibiti wa fedha ya kikundi |
| | (b) | Fedha yote kuwekwa benki |
| | (c) | Matumizi ya fedha |
| | (d) | Kusaini nyaraka za benki |
| | (e) | Idhini ya kutumia fedha ya kikundi |
| | (f) | Taarifa ya matumizi ya fedha |
| | (g) | Matumizi madogomadogo**(petty cash)** |
| | | **SEHEMU YA TANO** |
| **Ibara ya 15:** | | **UONGOZI WA KIKUNDI** |
| | (a) | Mwenyekiti |
| | (b) | Katibu |
| | (c) | Katibu Msaidizi |
| | (d) | Mhazini (Mweka Hazina) |
| | (e) | Kuchagua viongozi wa kikundi |
| **Ibara ya 16:** | | **VIKAO VYA KIKUNDI** |
| | (a) | Kikao cha kila mwezi |
| | (b) | Kazi za kikao cha kila mwezi |
| | (c) | Mkutano Mkuu |
| | (d) | Koramu ya mkutano mkuu |
| | (e) | Kazi za mkutano mkuu |
| | (f) | Uamuzi katika mkutano mkuu kupigiwa kura |
| | (g) | Kikao cha dharura |
| | (h) | Kupiga kura katika vikao |
| | | **SEHEMU YA SITA** |
| **Ibara ya 17:** | | **KUSITISHA SHUGHULI ZA KIKUNDI** |
| | (a) | Sababu za kusitisha kikundi |
| | (b) | Kikao kuidhinisha kusitisha kikundi. |
| | (c) | Kugawana fedha na mali baada ya kusitisha kikundi. |
| **Ibara ya 18:** | | **MAELEZO KUHUSU KATIBA HII** |
| | (a) | Kikundi kuendeshwa kwa mujibu wa katiba |
| | (b) | Tafsiri ya ibara katika katiba |
| | (c) | Kushughulikia maswala yasiooneshwa ndani ya katiba |
| | (d) | Kurekebisha katiba |
| | (e) | Mamlaka ya kuweka utaratibu na kanuni |

| | |
|---|---|
| **Ibara ya 19:** | **IBARA NYINGINEZO** |
| (a) | Uhuru binafsi kuheshimiwa |
| (b) | Kuondoa tofauti miongoni mwa wanakikundi |
| (c) | Uadilifu katika kuendesha kikundi |

..........................................................................................

# SEHEMU YA KWANZA

**Utangulizi**

**MSINGI WA KATIBA**

Sisi wenyeji wa Mbezi tunaoishi Mbezi Luis Dar es Salaam kwa kutambua umuhimu wa kushirikiana na kuunganisha nguvu, kwa dhati, tumeamua kuanzisha umoja wa kusaidiana.

Ibara ya 1:

**TAFSIRI YA MANENO**

Katika katiba hii, bila kuathiri maana kulingana na neno lilivyotumika ndani ya sentensi, maneno yafuatayo yatakuwa na maana ifuatayo:

**(a)** **Maafa:-**Tukio lolote baya lisilotazamiwa linaloweza kutia hasara ya mali au maisha na linaloweza kusababisha maumivu makali kwenye viungo vya Mwanadamu.

**(b)** **Mtoto:-**Mtoto wa Mwanakikundi mwenye jinsia ya kike au kiume aliye chini ya umri wa miaka 18.

**(c)** **Wategemezi:-** Watoto /ndugu wa Mwanakikundi anaoishi nao waliozidi umri wa miaka 18 na wasiozidi umri wa miaka 25 walioanishwa kwenye fomu ya Mwanakikundi.

**(d)** **Mlezi:-** Mtu anayewakilisha nafasi ya baba na mama aliyeanishwa kwenye fomu ya Mwanakikundi.

**(e)** **Mwaka wa kikundi:-**Utakuwa kuanzia wiki ya tatu ya Desemba mpaka wiki ya pili ya Januari ya mwaka unaofuata.

Januari mpaka Desembe

Ibara ya 2:

**UTAMBULISHO**

**(a)** **Jina la kikundi**

Jina la kikundi ni **UMOJA NI NGUVU**

**(b)** **Makazi ya kikundi**

Makazi ya kikundi yatakuwa Barabara ya Morogoro, Mbezi Luis Dar es Salaam. (ya Makabe) Nyumba namba 1110

**(c)** **Anuani ya Posta**

Anuani ya Posta ni S. L. P ~~32573~~, Dar es Salaam 10834

## SEHEMU YA PILI

Ibara ya 3:

**MADHUMUNI**

**(a)** **Kusaidiana katika matatizo**

(i) Kusaidiana katika misiba
(ii) Kusaidiana katika ugonjwa
(iii) Kusaidiana katika maafa
(iv) Kusaidiana katika shughuli za kijamii na uchumi.

**(b)** **Kushirikiana katika mambo mengine**

(i) Kushirikiana katika shughuli yoyote inayomhusu Mwanakikundi baada ya kutakiwa kufanya hivyo kama vile kujifungua, ubatizo, maulidi n.k kwa mujibu wa kanuni kwa kipindi husika.

(ii) Kujenga na kudumisha ushirikiano na mshikamano miongoni mwa wanakikundi.

Ibara ya 4: **MISIBA INAYOSTAHILI MSAADA**

**(a)** **Mwanakikundi**

Endapo Mwanakikundi atafariki, kiwango cha fedha kilichowekwa kutoka mfuko wa kikundi kitatolewa

**(b)** **Mke /Mume wa Mwanakikundi**

(i) Mke /Mume mmoja tu wa Mwanakikundi aliyeonyeshwa kwenye fomu maalumu ndiye atakayetambuliwa na kikundi, endapo atafariki, kiwango cha fedha kilichowekwa kitatolewa.

(ii) Endapo mke/mume anayetambuliwa na kikundi atafariki au kutalikiwa, yule atakayechukua nafasi yake ndiye atakayetambuliwa na kikundi.

**(c)** **Watoto wa Mwanakikundi**

(i) Watoto wa Mwanakikundi watakaotambuliwa na kikundi ni wale tu watakaokuwa wameainishwa kwenye fomu itakayojazwa na Mwanakikundi, na endapo mmoja wao atafariki kiwango cha fedha kilichowekwa kitatolewa.

(ii) Endapo mke/mume wa Mwanakikundi atafariki au kutalikiwa,watoto wake wataendelea kutambuliwa na kikundi

(iii) Endapo mke/mume aliyechukua nafasi ya mke/mume wa Mwanakikundi aliyetalikiwa au kufariki atazaa watoto na Mwanakikundi baada ya tukio la kifo au talaka,watoto hao watatambuliwa na kikundi

(iv) Endapo Mwanakikundi atakuwa na watoto wa kuzaa yeye wasiokuwa na mama au baba yao kutokana na kifo au talaka na watoto hao anaishi nao kwenye makazi yake, basi watoto hao watatambuliwa na kikundi.

**(d)** **Baba/Mama au Mlezi**

Baba/Mama au Mlezi wa Mwanakikundi akifariki kiwango cha fedha kilichowekwa kitatolewa kutoka kwenye mfuko wa kikundi.

**(e)** **Wategemezi**

Endapo mtegemezi wa Mwanakikundi atafariki, kiwango cha fedha kilichowekwa kitatolewa kutoka mfuko wa kikundi kama ilivyoainishwa 4(c) i.

ra ya 5: **AINA ZA MISIBA**

(a) **Misiba tofauti**

Endapo msiba utatokea kwa Mwanakikundi zaidi ya mmoja kwa kipindi kimoja, basi wote watapata fedha kutoka mfuko wa kikundi kusaidia misiba yao na Wanakikundi watajigawa sawa kuhudumia misiba hiyo.

(b) **Msiba mmoja wanakikundi tofauti**

Endapo msiba mmoja utatokea kwa Wanakikundi zaidi ya mmoja, kila Mwanakikundi atahudumiwa pekee na kupata kiwango cha fedha kutoka mfuko wa kikundi.

(c) **Misiba mingi Mwanakikundi mmoja**

Endapo Mwanakikundi atapata misiba zaidi ya mmoja katika tukio moja au katika wakati mmoja, hii itahesabika kama msiba mmoja isipokuwa kikao cha dharura kitajadili nyongeza ya huduma na pesa kulingana na uzito wa misiba hiyo.

(d) **Misiba mingi wakati tofauti**

Misiba iliyotokea kwa Mwanakikundi mmoja lakini kwa kupishana katika muda wa kutokea na kufanyika mazishi, hii itachukuliwa kama misiba tofauti na huduma itatolewa katika kila msiba.

(e) **Misiba mingi sehemu tofauti**

Endapo misiba miwili au zaidi itatokea kwa Mwanakikundi mmoja kwa wakati mmoja lakini sehemu tofauti, na misiba hiyo haiwezi kufanyika sehemu moja, huduma itatolewa katika kila msiba.

Ibara ya 6: **MIPAKA YA KUSAIDIANA KATIKA UGONJWA**

(a) **Mgonjwa aliyelazwa Hospitalini**

(i) Endapo mke/mume, mtoto au mtegemezi wa Mwanakikundi anayetambuliwa na kikundi kulingana na Ibara 4 ya katiba hii, atalazwa Hospitali kuanzia siku moja hadi wiki moja, kiwango cha fedha kilichopangwa pamoja na $^1/_3$ ya kiasi kilichopitishwa mara namba ya Wanakikundi wote kitatolewa kwenye mfuko wa kikundi.

(ii) Na endapo mgonjwa aliyetajwa katika (i) hapo juu ataendelea kulazwa Hospitali zaidi ya wiki moja, basi kila Mwanakikundi atawajibika kutoa mfukoni mwake ⅓ ya kiwango cha kila mmoja kama ilivyooneshwa hapo juu katika (i) kwa wiki tatu (3).

(iii) Na endapo mgonjwa aliyetajwa katika (i) hapo juu ataendelea kulazwa hospitalini zaidi ya mwezi itaundwa kamati ya kuratibu msaada kwa mgonjwa.

(b) **Mwanakikundi mgonjwa**

(i) Endapo Mwanakikundi atalazwa Hospitali, msaada utatolewa bila mabadiliko kama ilivyoonyeshwa katika Ibara ya 6(a) hapo juu

(ii) Endapo Mwanakikundi ataumwa kufikia hali ya kutojiweza, kila Mwanakikundi atawajibika kutoa mchango wa $^1/_3$ ya kiwango kilichoonyeshwa katika Ibara ya 6 (a) (ii) na (iii).

Ibara ya 7: **MIPAKA YA KUSAIDIANA KATIKA MAAFA**

Endapo Mwanakikundi atapata tukio la uharibifu wa mali au maisha lisilokuwa la kawaida wala kutazamiwa, kikao cha dharura, kitaitishwa ili kujadili jinsi ya kumsaidia pamoja na kupanga kiwango cha msaada.

**SEHEMU YA TATU**

Ibara ya 8: **WANAKIKUNDI**

(a) **Sifa za Mwanakikundi**

(i) Awe na umri usiopungua miaka 18

(ii) Awe na akili timamu

(iii) Awe na jinsia yeyote anayejiheshimu

(iv) Awe mkazi wa Dar Es Salaam

Awe mwanaume / mwanamke mwenye umri usiopungua miaka 18 anayekubaliana na katiba hii.

(b) **Ada kama sharti la Wanakikundi**

Pamoja na kutimiza sifa zote katika Ibara ya 8 (a), mtu yoyote hatahesabika kuwa Mwanakikundi mpaka atakapokuwa amelipa ada ya kiingilio pamoja na kuonyesha maendeleo mazuri katika mahudhurio, ulipaji wa ada za kila mwezi, kwa kufuata kanuni zitakazokuwa zimewekwa kwa kipindi hicho.

(c ) **Mwanakikundi mpya**

Mwanakikundi mpya, baada ya kutuma maombi na kutimiza masharti katika Ibara ya 8(a), atawajibika kulipa ada ya kiingilio ya wakati huo iliyowekwa na mkutano mkuu na kuonyeshwa kwenye kumbukumbu za kikundi, kwa kufuata kanuni zitakazokuwa zimewekwa kwa kipindi hicho.

Ibara ya 9: **HAKI ZA MWANAKIKUNDI**

(a) **Haki ya kusaidiwa**

Kila Mwanakikundi ana haki ya kusaidiwa kama ilivyoanishwa katika katiba hii.

(b) **Haki ya kukagua kumbukumbu**

Kila Mwanakikundi ana haki ya kukagua kumbukumbu na vitabu vya Kikundi baada ya kutoa notisi ya maandishi ya siku saba kwa katibu.

(c) **Haki ya kupewa maelezo**

Kila Mwanakikundi ana haki ya kuhoji na kupewa maelezo yanayohusu Matumizi ya fedha za kikundi.

(d) **Haki ya Kuongoza**

Kila mwanakikundi ana haki ya kuchagua/kuchaguliwa katika nafasi yeyote ya uongozi.

(e) **Haki ya Usawa**

Wanakikundi wote ni sawa na wanastahili msaada sawa bila upendeleo wala Ubaguzi.

Ibara ya 10: **WAJIBU WA MWANAKIKUNDI**

(a) **Kulipa ada**

Kila Mwanakikundi ana wajibu wa kulipa ada na michango kama ilivyoonyeshwa katika ibara ya 13 ya katiba hii.

(b) **Kulipa michango mingine**

Kila Mwanakikundi ana wajibu wa kulipa michango yoyote itakayoanzishwa chini ya Ibara 13(c) ya katiba hii.

(c) **Wajibu wakushirikiana**

Kila Mwanakikundi ana wajibu wa kushirikiana na Wanakikundi wenzake katika shughuli zote zinazohusu kikundi, kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 3(b)

(d) **Wajibu wa kulinda katiba**

Kila Mwanakikundi ana wajibu wa kuheshimu, kulinda na kutetea katiba hii.

(e) **Siri ya kikundi**

Masuala yote yanayohusu kikundi yatajadiliwa ndani ya kikundi na si vingenevyo na kila mwanakikundi ana wajibu wa kutunza siri ya kikundi.

Ibara ya 11: **KUJIONDOA AU KUVULIWA UANAKIKUNDI**

(a) **Kujiondoa mwenyewe**

(i) Mwanakikundi anaweza kujiondoa kwenye kikundi wakati wowote baada na kutoa notisi ya maandishi ya miezi mitatu

(ii) Endapo Mwanakikundi atajiondoa kwa hiari yake, hatarudishiwa michango yake yote.

(iii) Isipokuwa kama kujiondoa kwa Mwanakikundi kutasababishwa na ukiukwaji wa haki zake kikatiba, basi atarudishiwa michango yake kulingana na haki yake.

(b) **Kuhamia nje ya Dar es Salaam**

(i) Endapo Mwanakikundi atalazimika kuhamia nje ya Mkoa wa Dar es Salaam kulingana na majukumu ya kazi yake na hakuna jinsi yoyote ile ya kuendeleza uanakikundi wake, basi atarudishiwa michango yake kulingana na haki yake.

( c ) **Kifo cha Mwanakikundi**

(i) Endapo Mwanakikundi atafariki, basi haki yake katika kikundi atapewa mrithi wake aliyeainishwa kwenye fomu ya familia ya mwanakikundi.

(ii) Au Uanakikundi wake unaweza kuendelezwa na msimamizi wa mirathi au mrithi mkuu wa marehemu kwa maslahi ya familia ya marehemu isiyopanuka.Isipokuwa watoto wa marehemu watakaotimiza umri wa miaka 18 hawatachukuliwa kama sehemu ya familia ya marehemu

**(d) Kukiuka Katiba**

(i) Mwanakikundi anaweza kuvuliwa uanakikundi kama atakwenda kinyume na Katiba hii.

(ii) Isipokuwa hakuna Mwanakikundi yeyote atakayevuliwa Uanakikundi bila Kupewa haki ya msingi ya kujieleza ni kwa nini asivuliwe Uanakikundi.

(iii) Endapo Mwanakikundi atavuliwa Uanakikundi kwa kwenda kinyume na katiba hii,basi hatarejeshewa ada na michango yake yote.

**( e) Haki ya fedha ya Mwanakikundi**

Kwa kuondoa utata, haki ya fedha ya Mwanakikundi inaweza kupatikana Baada ya kutoa madeni ya jumla yanayodaiwa kikundi, kuongeza madeni Kinachodai kikundi, kugawa kwa Wanakikundi wote, kutoa deni binafsi Analodaiwa Mwanakikundi husika.

Ibara ya 12: **MUDA NA KIWANGO CHA MSAADA**

**(a) Muda wa kutoa msaada**

Kwa kuzingatia Ibara **ya 4, 5, 6 na 7** ya katiba hii msaada wa fedha na hali Utatolewa kwa Mwanakikundi aliyepatwa na matatizo mapema kadri inavyowezekana bila kuchelewa.

**Kiwango cha msaada**

(i) Kiwango cha fedha kwa ajili ya msaada kitapangwa na mkutano mkuu Kama ilivyooneshwa katika Ibara ya **16 e (ii)** ya katiba hii na kuwekwa kwenye kumbukumbu za kikundi.

(ii) Isipokuwa kiwango cha fedha kwa ajili ya msaada kinaweza kufanyiwa marekebisho kila mwisho wa mwaka ili kiende sambasamba na thamani halisi ya fedha.

## SEHEMU YA NNE

Ibara ya 13: **ADA NA MICHANGO**

**(a) Ada ya kiingilio**

Kila mtu anayekusudiwa kuwa Mwanakikundi atatakiwa kulipa ada ya kiingilio ambayo itapangwa na mkutano mkuu na kuwekwa kwenye kumbukumbu za kikundi

(b) **Ada ya kila mwezi**

(c) Kila Mwanakikundi atatakiwa kulipa ada ya kila mwezi ambayo kiwango chake kitapangwa na mkutano mkuu.

(d) **Ada nyinginezo**
Ada nyingine pamoja na viwango vyake vinaweza kuanzishwa na kupitishwa na mkutano mkuu
Viwango vya kiingilio, ada na michango mingine vitaainishwa kwenye kanuni za kikundi.

Ibara ya 14: **HAZINA**

(a) **Udhibiti wa fedha za kikundi**
Ada, michango pamoja na mapato yote ya kikundi yatakuwa chini ya udhibiti wa mweka hazina.

(b) **Fedha yote kuwekwa Benki**
Mweka hazina atawajibika kuweka fedha yote kwenye Akaunti ya kikundi kila mwezi.

(c) **Matumizi ya fedha**
Fedha ya kikundi itatumika kwa ajili ya kutekeleza majuku/madhumuni na matakwa ya kikundi tu.

(d) **Kusaini nyaraka za Benki**
Wanakikundi watachagua miongoni mwao watu wasiopungua wawili watakao saini nyaraka za Benki na kumbukumbu za uteuzi wao zitatunzwa.

(e) **Idhini ya kutumia fedha ya kikundi**
Bila kuathiri Ibara ya 16 (g) (iii) ya katiba hii, matumizi yoyote ya fedha ya kikundi pamoja na ruhusa ya kuchukua fedha kutoka Benki au hazina ya kikundi itaidhinishwa na kikao halali / dharura na kuwekwa kwenye kumbukumbu ikionyesha wazi:-

(i) Kiasi cha fedha kinachohitajika
(ii) Matumizi ya fedha hizo.
(iii) Tarehe ya kuidhinisha matumizi hayo.
(iv) Namba ya hundi au vocha itakayo/zitakazotumika na
(v) Salio la fedha zilizobaki.

(f) **Matumizi madogomadogo (Petty Cash)**
Mweka hazina atawajibika kuweka fedha yote katika akaunti ya kikundi isipokuwa anaruhusiwa kubaki na fedha kiasi (Petty cash) kwa ajili ya matuminzi ya dharura kama itakavyoainishwa kwenye kanuni.

( g ) **Taarifa ya matumizi ya fedha**
Mweka hazina atawajiba kuaandaa na kuwasilisha taarifa ya mapato na matuminzi kila baada ya miezi mitatu na kila mwisho wa mwaka wa kikundi akiambatanisha na taarifa ya Benki (Statiment ya Akaunti ya kikundi).

## SEHEMU YA TANO

Ibara ya 15: **UONGOZI WA KIKUNDI**

**(a)** **Mwenyekiti**

(i) Atakuwa kiongozi mkuu wa shughuli za kikundi na ataendesha vikao vyote vya kikundi.Isipokuwa uamuzi wote wataachiwa wanakikundi wenyewe.

(ii) Atachaguliwa miongoni mwa Wanakikundi na kushika nafasi hii kwa kipindi cha miaka miwili isipokuwa anaweza kugombea tena nafasi hii kwa mujibu wa kanuni.

(iii) Nafasi ya Mwenyekiti inaweza kukaimiwa na Mwanakikundi yeyote atakayeteuliwa kufanya hivyo na Wanakikundi wenzake.

(iv) Mwenyekiti anaweza kuondolewa kwenye Uongozi baada ya kushindwa kulinda katiba, na kuwa na matatizo ya afya na akili.

**(b)** **Katibu**

(i) Atakuwa Mwandishi mkuu na mtendaji mkuu wa kikundi

(ii) Atakuwa mtunzaji mkuu wa nyaraka na kumbukumbu zote za kikundi.

(iii) Atakuwa mtoaji na mpokeaji mkuu wa habari miongoni mwa Wanakikundi na kuhusu shughuli za kikundi na matatizo ya Wanakikundi.

(iv) Atachaguliwa miongoni mwa Wanakikundi na kushika nafasi hii kwa kipindi cha miaka miwili, isipokuwa anaweza kugombea tena nafasi hii kwa mujibu wa kanuni.

(v) Katibu anaweza kuondolewa kwenye nafasi yake iwapo atakwenda kunyume na katiba hii au kuwa na matatizo ya akili au afya.

**(c)** **Katibu Msaidizi**

Atafanya kazi zote za katibu / mhazini watakapokuwa hawapo.

**(d)** **Mweka Hazina**

(i) Atakuwa mpokeaji wa ada na michango yote pamoja na kudhibiti mapato yote ya kikundi

(ii) Atakuwa mlipaji na mpelekaji fedha Benki au mchukuaji fedha kutoka Benki pamoja na kushughulikia hundi na nyaraka zote za Benki.

(iii) Atachaguliwa miongoni mwa Wanakikundi na kushika nafasi hii kwa kipindi cha miaka miwili, isipokuwa anaweza kugombea tena nafasi hii kwa mujibu wa kanuni.

(iv) Mweka hazina anaweza kuondolewa kwenye nafasi yake iwapo ataenda kinyume na kazi yake au kushindwa kumudu kazi yake kutokana na matatizo ya akili au afya.

**(e) Kuchagua viongozi wa kikundi**

(i) Kila Mwanakikundi katika mkutano mkuu atachagua jina la Mwanakikundi yoyote kwa siri katika nafasi husika kama ilivyo katika ibara ya **15 a, b na c,** atakayepata kura nyingi atapitishwa kushika nafasi husika.

## Ibara ya 16: VIKAO VYA KIKUNDI

**(a) Kikao cha kila mwezi**

(i) Kikao cha kila mwezi kitafanyika kila Jumapili ya katikati ya mwezi saa 10 jioni.

(ii) Kikao cha kila mwezi kitafanyika katika mojawapo ya makazi ya Mwanakikundi.Utaratibu wa mahali pa kufanyia kikao utapendekezwa na Wanakikundi na endapo mhusika hatakuwepo kutokana na dharura Wanakikundi wataamua sehemu nyingine ya kufanyia kikao.

(iii) Kikao cha kila mwezi kitaanza baada ya zaidi ya nusu ya Wanakikundi wote kuhudhuria ikiwa ni pamoja na walioomba udhuru.

**(b) Kazi za kikao cha kila mwezi**

(i) Kutathimini shughuli za kikundi kwa mwezi husika

(ii) Kutathimini maendeleo ya michango

(iii) Kubuni mikakati mbalimbali ya kuendeleza na kudumisha kikundi

**(c) Mkutano mkuu**

Mkutano mkuu utafanyika mara moja kila mwaka, baada ya mwaka wa kikundi kukamilika katika sehemu itakayopendekezwa na Wanakikundi.

**(d) Koramu ya mkutano mkuu**

Mkutano mkuu unaweza kufanyika baada ya kuhudhuria robo tatu ya Wanakikundi wote pamoja na watakaoomba udhuru.

**(e) Kazi za mkutano mkuu**

(i) Kutathimini shughuli za kikundi kwa kipindi cha mwaka husika

(ii) Kuweka na kurekebisha viwango vya ada, michango na misaada kama kutakuwa na umuhimu wa kufanya hivyo

(iii) Kwa kuzingatia Ibara ya 18(d) ,mkutano mkuu unaweza kurekebisha Katiba hii kama kutakuwa na umuhimu wa kufanya hivyo.

( iv ) Kwa kuzingatia Ibara ya 18(e) ,mkutano mkuu unaweza kuweka utaratibu na kanuni za kuendesha kikundi

( v) Kupanua wigo wa madhumuni na kuongeza au kupunguza madhumuni ya kikundi

(vi ) Kufanya uchaguzi wa viongozi wa kikundi.

VII Kujadili mwenendo wa Wanakikundi na Kutoa maamuzi Kama itakavyowasilishwa na Uongozi

(f) **Uamuzi katika mkutano mkuu**
Uamuzi wowote ule utapitishwa na mkutano mkuu baada ya kuungwa mkono na zaidi ya nusu ya Wanakikundi waliohudhuria

(g) **Kikao cha dharura**

(i) Kikao cha dharura kinaweza kufanyika kama Mwanakikundi yeyote,au Wanakikundi baada ya kutoa notisi ya siku tatu kwa katibu ikionyesha Sababu ya kuitishwa kwa kikao cha dharura.Katibu atawajulisha Wanakikundi agenda, tarehe muda na sehemu ya kufanyika kikao hicho

(ii) Kikao cha dharura kinaweza kuitishwa kama litatokea tatizo lolote kama Msiba n.k katika hali hii notisi haitahitajika, isipokuwa katibu atawajibika kutoa taarifa kwa Wanakikundi wote.

(iii) Endapo kikao cha dharura kitaitishwa kwa ajili ya kujadili msiba n.k kama inavyoelezwa hapo juu, Wanakikundi walioweza kukusanyika kwa kuzingatia katiba, wanaweza kutoa uamuzi mapema na haraka iwezekanavyo kutatua tatizo.Kama katibu hatakuwepo basi taarifa zipelekwe kwa kiongozi yeyote atakayepatikana.

Kiondolewe.

(h) **Kupiga kura katika vikao**

(i) Endapo kutakuwepo na mvutano katika kufikia uamuzi katika vikao, basi kura ya siri itapigwa na mwenyekiti atakuwa na kura ya turufu.

(ii) Katika hesabu ya kura Baba na Mama watakuwa na kura moja tu.

## SEHEMU YA SITA

Ibara ya 17: **KUSITISHA SHUGHULI ZA KIKUNDI**

(a) **Sababu za kusitisha kikundi**.
Endapo kutatokea hali yoyote ile isiyotazamiwa ambayo kwa njia yoyote ile shughuli za kikundi haziwezi kuendelea,basi kikundi kitasimamisha shughuli zake.

(b) **Kikao kuidhinisha kusitisha kikundi**
Shughuli za kikundi zitasitishwa rasmi baada ya kikao cha dharura kikiwa na Wanakikundi wasiopungua robo tatu, kupitisha usitishaji wa shughuli za kikundi

(b) **Kugawana fedha na mali baada ya kusitisha**
Endapo kusitishwa kutaidhinishwa, fedha pamoja na mali ya kikundi,baada ya kulipa madeni yote,zitagawiwa miongoni mwa Wanakikundi kulingana na haki ya kila mmoja

Ibara ya 18: **MAELEZO KUHUSU KATIBA HII**

(a) **Kikundi kuendeshwa kwa mujibu wa katiba**
Kikundi kitaendeshwa kwa mujibu wa katiba hii kanuni na taratibu zilizowekwa.

(b) **Tafsiri ya Ibara katika katiba**
Lugha na maana ya maneno yaliyotumika katika katiba hii yatatafsiriwa kama yalivyo, isipokuwa pale penye utata patapewa tafsiri nzuri isiyokusudia kumpokonya Mwanakikundi yeyote haki yake.

(c) **Kushughulikia masuala yasiyooneshwa ndani ya katiba**
Endapo suala lolote litajitokeza ambalo halikuonyeshwa katika katiba hii litajadiliwa na Wanakikundi na kupewa fumbuzi.Isipokuwa pengo hilo halitazibwa kwa kumpokonya Mwanakikundi yeyote haki yake.

(d) **Kurekebisha katiba**

(i) Marekebisho ya katiba hii yanaweza kufanywa na mkutano mkuu baada ya Wanakikundi kuamua kufanya hivyo. Wakati wowote ule na kikao cha dharura cha kurekebisha katiba

(ii) Isipokuwa hakuna marekebisho ya katiba yatakayofanyika kugeuza kipengere chochote kwa nia ya kumpokonya Mwanakikundi yeyote haki yake.

(f) e **Mamlaka ya kuweka utaratibu na kanuni**
Bila kuathiri katiba hii, mkutano mkuu utakuwa na mamlaka ya kuweka utaratibu na kanuni za kuendesha kikundi.Isipokuwa hakuna utaratibu au kanuni zitakazotumika bila kukubaliwa na robo tatu ya Wanakikundi wote.

Ibara ya 19: **IBARA NYINGINEZO**

(a) **Uhuru binafsi kuheshimiwa**

(i) Uhuru binafsi wa Mwanakikundi utaheshimiwa wakati wowote wa utekelezaji wa shughuli za kikundi,

(ii ) Mwanakikundi yeyote ana haki ya kufanya mambo yake bila kuingiliwa na Wanakikundi wengine, ili mradi kwa kufanya hivyo hakuathiri shughuli za kikundi.

(b) **Kuondoa tofauti miongoni mwa wanakikundi**
Endapo kutatokea tofauti yoyote miongoni mwa Wanakikundi kuhusu shughuli za kikundi, tofauti hiyo itajadiliwa na kuondolewa na Wanakikundi wenyewe kwa kutumia busara, hoja, hekima na usitahimilivu.

(c) **Uadilifu katika kuendesha kikundi**

Shughuli zote za kikundi zitaendeshwa kwa upendo, uwazi uaminifu na uadilifu mkubwa.

(d) Kwa kuwa kikundi hiki hakiendeshwi kwa misingi ya dini / kabila, kila shughuli za kikundi zitaanza kwa dua ifuatayo;

**"EWE MUNGU MWENYEZI, ULIYE MPAJI WA MEMA YOTE; TUNAKUOMBA,SISI TULIOUNGANIKA KATIKA UMOJA NI NGUVU,KWA NIA YA KUJILETEA MAENDELEO NA KUSAIDIANA KATIKA KUYAKABILI MAWIMBI MBALMBALI YA MAISHA YA ULIMWENGU HUU;UTUJALIE BUSARA, HEKIMA, UVUMILIVU, UPENDO NA MAFANIKIO KATIKA KUJADILI YOTE YALIYO MBELE YETU. TUNAKUOMBA UTUWASHIE MWANGA KATIKA UCHAMBUZI NA UFAFANUZI ILI MAAMUZI TUTAKAYOYAFANYA YAWE YA KUFANIKISHA NIA ZETU NA UTUKUFU WAKO."**

AMINA

**T A M A T I**

# MUNGU KIBARIKI KIKUNDI CHETU.